

HOTUBA JUU YA WARSHA YA MAHITAJI NA VIKWAZO KATIKA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA KIFEDHA NCHINI TANZANIA

Kwa miaka ya hivi karibuni huduma za kifedha zimeonekana kushamiri sana katika sehemu mbalimbali kuashiria kuwa ni za muhimu kwa wananchi wa sehemu yoyote duniani. Uwekaji wa akiba pamoja na uchukuaji wa mikopo vimekuwa ni vitu vya muhimu sana katika maisha na maendeleo ya watu na nchi kwa ujumla. Kufuatia umuhimu huu mwaka 2009, Benki Kuu ya Tanzania ikishirikiana na Mfuko wa Kuboresha Huduma za Kifedha nchini uitwayo Financial Deepening Trust Fund (FSDT) iliendesha utafiti ujulikanao kama FinScope ambao ulilenga Katika kupata hali halisi kitaifa na kimikoa juu ya mitazamo ya watumiaji kuhusu mahitaji na vikwazo vinanyokinza upatikanaji wa huduma za kifedha Tanzania Bara na Visiwani.

Utafiti wa FinScope 2009 ni utafiti wa pili kufanyika Tanzania ambapo wa kwanza ulifanyika mwaka 2006. FinScope 2009 ilihusisha sampuli ya watu wapatao 7,680 iliyoainishwa na Idara ya Takwimu ya Taifa (NBS) na iliwakilisha uwiano halisi wa idadi ya watazania bara na visiwani. Kitakwimu maeneo yote yaliyohusishwa katika utafiti huu (Kitaifa na mikoa) yaliwakilishwa kwa uwiano uliokuwa sawa.

Katika kuchambua matokeo haya, Taasisi ya Utafiti juu ya masuala ya kiuchumi na kijamii Tanzania (ESRF) na kampuni ya ushauri wa masuala ya maendeleo (DPC) mwaka 2010, waliandaa warsha mbalimbali zinazoendelea nchi nzima kusambaza matokeo haya na kutoa ushauri na uchambuzi yakinifu kuhusiana na takwimu za utafiti wa FinScope 2009. Kama itakavyoonyeshwa katika Warsha hii, lengo kuu la Utafiti huu ni kutoa msaada kwa serikali, watunga sera, watoa huduma za kifedha kwenye mabanki, taasisi binafsi, watafiti, wasomi na jumuiya ya wafadhili kwa ujumla juu ya uelewa, mahitaji na matumizi ya huduma hizi nchini na kuonyesha changamoto zilizopo katika upatikanaji wa huduma hizi kwa walengwa. Hivyo umelenga katika kuisaidia serikani namna ambavyo

inaweza kuyasimamia mashirika ya kifedha kuweza kuwafikia wananchi wote na kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kutumia huduma zitolewazo na vyombo hivi kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi katika ngazi ya kaya, wilaya, mkoa na taifa kwa ujumla.

Warsha hii ya leo, inakutanisha wafanyakazi wa serikalini ngazi ya mkoa na wilaya, taasisi mbalimbali zinazohusika na utafiti nchini na vyuo vya elimu ya juu kutoka mikoa ya Arusha, Manyara, Singida na Kilimanjaro. Kwa hiyo mwisho wa warsha hii inategemewa kuwa washiriki wote mlialikwa hapa mta elewa juu ya sababu za kanda hata za mtu binafsi kutumia au kutotumia huduma za kifedha, vikwazo vya upatikanaji wa huduma hii na pia kujua fursa zilizopo ili kuweza kuongeza matumizi ya huduma hizi katika maeneo yenu na nchini kwa ujumla. Hivyo basi kama washirika tunaombwa tuwe makini wakati wa warsha hii na ikibidi tushiriki kikamilifu na kutoa maoni juu ya njia mbalimbali ambazo zinaweza kusaidia kuboresha upatikanaji na utumiaji wa huduma hizi nchini.

Kwa kweli tunawashukuru ESRF,DPC na FSĐT kwa kuweza kutuletea taarifa muhimu za utafiti walioufanya na huu ni mfano mzuri kwa vyombo vingine vinavyofanya utafiti kuweza kurudisha majibu kwa walengwa ili kutumia majibu ya utafiti kwa maendeleo ya nchi. Asanteni sana.

Kwa haya machache ningependa kusema kuwa warsha hii imefunguliwa rasmi na karibuni sana.

AKSANTENI.